DIOCESE OF CENTRAL TANGANYIKA
MVUMI SECONDARY SCHOOL

Phone: 0732- 961171
Website: www.dctmvumi.sc.tz
Email: info@dctmvumi.sc.tz

Headmaster's Phone: 0714-278470
E-mail: headmaster@dctmvumi.sc.tz
P.O.Box 62, Mvumi, Dodoma

Ref: DCT/MSS/JI/2022/1 Tarehe: _____

FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023
WANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI

Ndugu Mzazi/Mlezi wa _____tunayo furaha kukujulisha kuwa kijana wako amechanguliwa kujiunga na shule yetu katika mchepuo wa Masomo ya _____ kuanzia Jumatatu ya tarehe **30/05/2022.** Mwanafunzi wa Bweni atatakiwa kuripoti siku ya Jumapili ya tarehe **29/05/2022** kuanzia saa **3:00 asubuhi** hadi saa **12:00 jioni.**

1. Shule iko kijiji cha **Mvumi Mission** katika wilaya ya **Chamwino** umbali wa kilometa 40 kusini mwa Mji wa Dodoma. Usafiri unapatikana stendi ya Mvumi iliyopo Majengo Dodoma mjini muda wote asubuhi mpaka **j**ioni.

2. Vifaa vyote vilivyo orodheshwa kwenye fomu hii vitakaguliwa shuleni kwa wanafunzi wote wa bweni na kutwa watakapokuwa wamefika shuleni. Mwanafunzi yeyote ambaye hatakamilisha mahitaji yote yalioorodheshwa, **HATAPOKELEWA!**

3. Sheria na taratibu za shule zimeambatishwa.(mzazi unashauriwa kutoa kivuli cha sheria za shule na kubaki na nakala yako kwa kumbukumbu).

4. Tarehe ya mwisho ya kuripoti shuleni ni wiki moja baada ya kufungua shule ambayo ni tarehe **06/06/2022** baada ya hapo nafasi atapewa mwingine na ada **HAITARUDISHWA.**

Yafuatayo ni mahitaji ya shule anayotakiwa mwanafunzi atimiziwe ili aweze kukubaliwa kujiunga na shule. **Kwa vile vilivyoainishwa kuwa vinapatikana katika Duka la Shule vinunuliwe toka Duka la Shule vinginevyo havitapokelewa.**

A. SARE YA SHULE NA VIFAA VYA MICHEZO

WASICHANA

i) Sketi mbili za rangi ya kijivu zenye marinda ya kupanga na urefu wa kupita magotini.
ii) Mashati mawili meupe mikono mirefu.
iii) Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu na sio travota.
iv) Raba za michezo jozi moja au zaidi kulingana na aina ya michezo anayocheza

WAVULANA

i) Suruali mbili za rangi ya kijivu isiyo jeans.
ii) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu jozi mbili
iv) Raba za michezo jozi moja au zaidi kulingana na aina ya michezo anayocheza

Sare ya Shule na Vifaa vya michezo vifuatavyo mwanafunzi atapewa shuleni kwa gharama elekezi ambayo ni **263,100/= kwa Washichana** na **281,100/= tu kwa Wavulana. Gharama hii mzazi alipie benki kwenye akaunti ya shule ya NMB pekee na si vinginevyo.**

Akaunti Na: 52010017604

Jina la Akaunti: D.C.T Mvumi Secondary School

ZINGATIA: Gharama tajwa hapo juu iwe imeshalipwa kabla ya tarehe 30/05/2022. Vinginevyo mwanafunzi hatapokelewa.

SARE YA SHULE, VIFAA VYA MICHEZO, VIFAA VYA TAALUMA na VIFAA VYA BWENI					
WAVULANA		**GHARAMA**	**WASICHANA**		**GHARAMA**
1	T- Shirt	13,000	1	T-Shirt	13,000
2	Sweater (Yenye nembo ya shule)	14,000	2	Sweater *(Yenye nembo ya shule)*	14,000
3	Soksi Jozi 02 Nyeusi *(ndefu)*	5,000	3	Soksi Jozi 02 Nyeupe *(ndefu)*	5,000
4	Kitambulisho	10,000	4	Kitambulisho	10,000
5	Jezi	15,000	5	Jezi	15,000
6	Track – Suit	28,000	6	Track - Suit	28,000
7	Mkanda wa suruali	7,000	7	Soksi za michezo 02	10,000
8	Soksi za michezo 02	8,000	10	Mkebe wenye vifaa vya hisabati	2,000
9	T-shirt ya kushindia *(Form six)*	15,000	11	Karatasi za photocopy (Ream 1)	18,000
10	Mkebe wenye vifaa vya hisabati	2,000	12	Counter Book Q3 matano	12,500
11	Karatasi za photocopy (Ream 1)	18,000	13	Penceli @	300
12	Counter Book Q3 matano	12,500	14	Peni @	300
13	Penceli @	300	15	Godoro la 3½" x 6 (Imara)	75,000
14	Peni @	300	16	Mashuka mawili ya pamba	15,000
15	Godoro la 3½" x 6 (Imara)	75,000	17	Ndoo ndogo lita 10	3,000
16	Mashuka mawili ya pamba	15,000	18	Mswaki na dawa ya mswaki	1,500
17	Ndoo ndogo lita 10	3,000	19	Dawa ya viatu na brush	3,000
18	Mswaki na dawa ya mswaki	1,500	20	Sabuni za kuogea na kufulia	2,000
19	Dawa ya viatu na brush	3,000	21	Pedi	2,000
20	Sabuni za kuogea na kufulia	2,000	22	Chandarua 4 x 6	10000
21	Chandarua 4 x 6	10000	23	Kufuli moja	2500
22	Kufuli moja	2500	24	Kwanja, Jembe na Fagio la Chelewa	16000
23	Kwanja, Jembe na Fagio la Chelewa	16000	25	Sahani, bakuli, kikombe na kijiko	5000
24	Sahani, bakuli, kikombe na kijiko	5000			
	JUMLA	**281,100**		**JUMLA**	**263,100**

B. SARE MAALUM

(i) Nguo za kushindia baada ya masomo zitakuwa kama ifuatavyo;

- Kwa wasichana watatakiwa kuvaa gauni refu la damu ya mzee lililoshonwa kwa mshono wa solo. **(Aje nalo)**
- Wavulana watatakiwa kuvaa suruali za rangi nyeusi **(Aje Nayo)** na Tshirt damu ya mzee **(inayopatikana kwenye duka la shule).**

Mwanafunzi hataruhusiwa kuja na nguo za kuvaa baada ya masomo ambazo hazijaorodhesha kwenye fomu hii.

C. VIFAA VYA TAALUMA

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo na vinapatikana kwenye Duka la Shule

i) Vitabu binafsi kulingana na mchepuo wa masomo husika.
ii) Kikokotozi cha mahesabu (Silent non-programmable calculator with functions ranging from fx -82MS to fx-991MS) kwa wale wanaochukua michepuo inayohusisha hisabati.
iii) Saa ya mkononi ni lazima kwa kila mwanafunzi.
iv) Begi imara na salama la kubebea madaftari na vitabu ni lazima kwa kila mwanafunzi.

D. PICHA ZA PASSPORT SIZE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwasilisha ofisi ya taaluma nakala nne za picha za passport size za rangi *(Zipigwe akiwa amevaa shati jeupe).*

E. VIFAA VIFUATAVYO NI LAZIMA KWA MWANAFUNZI KUWA NAVYO.

1. Trunker
2. Blanketi moja.
3. Mto (pillow)
4. Taulo (Towel)

MUHIMU

- Matibabu yatagharamiwa na mzazi nje ya ada. Unashauriwa kuleta **shs 30,000** au zaidi kila muhula kwa ajili ya matibabu ambazo zitahifadhiwa na shule na kutumiwa na mwanafunzi kwa ajili ya matibabu pindi auguapo. AU Mzazi/Mlezi Unashauriwa kumkatia bima ya afya **(NHIF)** mwanao kwa gharama **50,400/=.**
- Shule haina Utaratibu wa kutoa chakula special kwa wanafunzi wenye matatizo mabalimbali ya kiafya. Gharama hizo zitagharamiwa na mzazi au mlezi wa mwanafunzi husika.

I. MCHANGANUO WA MALIPO YA ADA (KARO) MWAKA 2022/2023

S/NO.	TAREHE	KUTWA	BWENI
1.	May, 2022	700,000/=	1,300,000/=
2.	January, 2023	600,000/=	1,200,000/=
	Jumla	**1,300,000/=**	**2,500,000=**

Malipo ya ada **LAZIMA** yafanyike benki kulingana na jedwali hilo hapo juu vinginevyo mwanafunzi hataruhusiwa kuendelea na masomo hapa shuleni, mzazi/mlezi unashauriwa kutimiza wajibu wako wa kulipa ada bila kukosa ili kutokusababisha usumbufu kwa mwanao.

CRDB Bank Akaunti Namba: 0150447830600

Jina la akaunti: D.C.T Mvumi Secondary School.

<u>Jina la mwanafunzi na kidato liandikwe kwenye pay in slip (fomu ya kuweka fedha)</u> na mwanafunzi aje nayo anaporipoti shuleni). ADA IKISHALIPWA HAIRUDISHWI (NON-REFUNDABLE)

<u>ZINGATIA:</u> Ada iwe imeshalipwa kabla ya tarehe 30/05/2022. Vinginevyo mwanafunzi hatapokelewa.

F. URAIA

Ili kuthibitisha uraia wa mtoto wako unatakiwa kuleta kivuli (photocopy) cha cheti cha kuzaliwa au hati ya kiapo kutoka mahakamani (Affidavit).

G. AFYA

Mtoto wako atatakiwa kuchunguzwa afya yake katika Hospitali ya ngazi ya Wilaya au Mkoa na kujaza fomu iliyoambatishwa (Medical Examination Form), pia kuweka sahihi na muhuri wa Mganga Mkuu wa Hospitali husika.

Wako katika kazi,

HEADMASTER
D.C.T. MVUMI SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 62, MVUMI - DODOMA

Kwa mawasiliano tumia namba za simu zifuatazo:

- **0714 – 278 470 Mkuu wa Shule (Head of School)**
- **0717- 129 355 Makamu Mkuu wa Shule (Deputy Head of School)**
- **0713 - 307 671 Karani wa Mkuu wa Shule (Headmaster's Secretary)**

ORODHA YA VITABU VYA MASOMO KWA A-LEVEL

(Mzazi/ Mlezi unashauriwa kumnunulia kijana wako VITABU binafsi kulingana na mchepuo wa masomo anaosoma)

SOMO LA PHYSICS

1. Principles of physics class XI; S. Chand
2. Principles of physics, class XII; S. Chand
3. Principles of Physics; Nelkon and Parker.
4. Advanced Level physics 4th edition; Roger Muncaster
5. Advanced Level physics 5th edition; Tom Duncan,
6. Physics review question paper I and II; APE Networks

SOMO LA CHEMISTRY

1. Advanced chemistry; Philip Mathews, Low price edition
2. Physical chemistry, by Delungu (Mzumbe bookshop project 1998)
3. Advanced inorganic chemistry part I and II (Tanzania institute of education).
4. Organic Chemistry part 1, The fundamental principles I.L finar (longman LTD)

SOMO LA GEOGRAPHY

1. Principles of physical geography by F J monk house
2. Geography integrated approach by D.waugh
3. Essentials of Practical Geography by Josephat Mwita
4. General geography in diagram by R B burnet
5. Simplified physical Geography(A-LEVEL) by D M
6. Statistical methods and the geographers by s. Gregory
7. Geography for Advanced Level 1 & 2 (Tanzania institute of education)

SOMO LA BIOLOGY

1. Biological science 1 &2; Cambridge university press 1997, 3rd edition
2. New Understanding Biology; 4th edition Suzan Toole
3. Advance biology Principles and application By C J Clegg and Mackean
4. Advanced Biology; Michael kent (2000). Oxford university press Uk.

SOMO LA ADVANCED AND BASIC APPLIED MATHEMATICS

1. Basic applied Mathematics for secondary school, Book V and VI; by Kiza and Septine I sillem
2. Advanced Mathematics; Shayo
3. Advanced Mathematics book 1 and 2; Backhouse
4. Advanced Mathematics 1 and 2; S. Chand

SOMO LA HISTORY

1. Advanced learners, History form V and VI (history 1 and 2)(oxford 2011)
2. Essentials in advanced level history paper 1; Salen Yassin
3. Essentials in advanced level history paper 2; Salen Yassin
4. Basic themes in advanced level history, Paper 1; F.M Mavunde
5. Advanced level History for Africa, From Neolithic Revolution to present;(zist Kamili 2010)
6. Focus on Modern world history by Japhace, Ponsian, Chakupewa, Mpandije Yusuph P Maunda (2012

SOMO LA ENGLISH

1. Oxford University Press (2014). Advanced English Language Forms 5 and 6: Dar es Salaam. Oxford University press Ltd.
2. Kadeghe, M (2010). The real English Form Five, Jamana Printers
3. Kadeghe, M (2010). The real English Form Six, Jamana Printers
4. Asheli, N (2010). Advanced level English, Good Books Publishers.
5. Nyangwine N &Bukagile G,R.(2008). Advanced Level Literature.Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
6. Hornby, A.S. (2006). Oxford Advanced Learner's Dictionary 7th Edition.Oxford: Oxford University Press.
7. Macmillan Education Ltd (2000). Encounters from Africa, Macmillan
8. Ayi Kwei Amah, (1996). The beautiful ones are not yet born, EAEP
9. Chinua Achebe, (1991). A man of the people, BAEP
10. Ndunguru (1999). Divine Providence, mkuki na nyota
11. Magala Nyago, (1985). The Rape of the Pearl Macmillan
12. Namige Kayondo, (1995). Vanishing shadows, Macmillan
13. Danny Sato, (1983). His Excellency the head of state, Macmillan
14. David Omowale, (2002). A season of waiting, EAEP
15. Francis Imbuga, (1990). Betrayal in the city, Heinemann
16. Ngugi wa Thiong'o, et al (1982). I will marry when I want, EAEP
17. Bukenya A, (1984). The Bride, EAEP
18. Okoit Omtatah, (1991). Lwanda Magere Heinemann
19. Henrick Ibsen, (1974). An Enemy of the people, Eyre Matheuen
20. John Ruganda, (2005). Black Mamba, EAEP
21. Charles Mloka, (2002). The wonderful surgeon and other poems, Mkuki na Nyota
22. Tanzania Institute of Education, (1996). Selected poems, Print pak (t) Limited.

SOMO LA KISWAHILI

1. Nadharia ya lugha, kidato cha 5 &6; J.A MASEBO etal
2. Nadharia ya fasihi, kidato Cha 5 & 6; J.A MASEBO etal
3. Tahakiki vitabu teule vya fasihi kidato cha 5 &6; J.A MASEBO, etal
4. Kiswahili 1& 2; M. SALUHAYA
5. Jitayarishe kwa fasihi ya Kiswahili; nyambari etal

SOMO LA GENERAL STUDIES

1. General studies for a level; Z. KAMILI. 2017 edition
2. General studies supplementary book for A- level and colleges. By Konrad Adenauer
3. Understanding General Studies for Advanced Level by Joannes Bigiramungu & Sospeter Deogratius.

ECONOMICS

1. Economics Theory by Gupta
2. Micro-economics by Dwiverd
3. Modern economics By Robert Mudida
4. Economic simplified East Africa Edition by N.A Saleem.
5. Principle of Economics by M. L. Jinghan
6. Advanced Economy Book 1 & 2 Ambilikile C (2009)
7. Modern-Micro Economics by Chand S
8. Economics by Zist Kamili

MUHIMU

- Somo la General Studies (GS) litasomwa na wanafunzi wote kwa michepuo yote.
- Somo la Basic Applied Mathematics (BAM) litasomwa na wanafunzi wote wa PCB, CBG, na HGE.
- Mwanafunzi anaruhusiwa kuja na vitabu vingine au study material zingine zitakazomsaidia kufanya vizuri katika masomo yake, i.e past papers, past notes etc.

FORM: F 1.1

DIOCESE OF CENTRAL TANGANYIKA
MVUMI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 62,
MVUMI

TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

1. JINA: _____ JINSIA: _____

TAREHE YA KUZALIWA: _____

ANUANI: _____

_____

2. SHULE ALIYOSOMA O-level:_____

MKOA ILIPO SHULE:……..WILAYA:…….

NAMBA YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA NNE: _____

UFAULU KIDATO CHA NNE: DARAJA**(Division)**: ……..... POINTI: ……

TAHASUSI ULIYOPANGIWA: ……UFAULU KWENYE TAHASUSI NI KAMA IFUATAVYO:

Ujazaji kipengele (a) ni mfano na (b) ni halisi kijazwe na mwanfunzi		Mfano; mwanafunzi (X)aliyepangwa **PCB** ufaulu wake O-Level masomo ya Tahasusi tajwa hapo juu ni kama:-			JUMLA YA POINTI ZA TAHASUSI
(a)Mfano	SOMO	PHYSICS	CHEMISTRY	BIOLOGY	PCB
	UFAULU	A	B	C	06
(b)JAZA HAPA(ufaulu wako)	SOMO				
	UFAULU				

Ufunguo:- A=1,B=2,C=3,D=4, F=5.

3. Unapenda kusomea Fani gani utakapojiunga na Elimu ya Juu? Mf. SHERIA, MWALIMU n.k

_____

4. JINA LA BABA:_____

KAZI:_____ ANUANI: _____

JINA LA MAMA: _____

KAZI: _____ANUANI: _____

JINA LA MLEZI: _____

KAZI: _____ANUANI: _____

SIMU: _____

KABILA: _____

MKOA: _____

WILAYA: _____

TARAFA: _____

KATA: _____

KIJIJI/MTAA: _____

DINI: _____

DHEHEBU: _____

5. Orodha ya Ndugu zangu ambao watakuwa wakinitembelea shuleni ni:

1. Jina:……...…Simu:……..

2. Jina:……..…….Simu:……..

3. Jina:……..…….Simu:……..

4. Jina:……..…….Simu:……..

DCT MVUMI SECONDARY SCHOOL
EDUCATION IS LIBERATION

FORM: F 1.2

DIOCESE OF CENTRAL TANGANYIKA
MVUMI SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 62, MVUMI
DODOMA

REF: MEDICAL EXAMINATION FORM

NAME: _____ DATE: _____
(Full name in capital letters with initial inserted)

Has undergone thorough medical examination.
By: .....(Doctor's name)

Of: ..... (Health Centre/Hospital)

Medical investigation details:

A. Blood analysis..... .....

....

B. Stool analysis ....

....

C. Urine analysis ....

....

D. Other ....

....

Recommendations: I ..... have thoroughly investigated the named person and do declare that he/she is physically fit/unfit to pursue studies.
If unfit, please state illness/infections/infection/other problems.....

Any physical disabilities YES/NO

If yes state type of disability: .....
Doctor's Name: ..... Signature: .....
Official stamp…….…….....

Date:.....
Return duly filled form to the **HEADMASTER**

Mimi(Mwanafunzi) ……bila kushinikizwa na mtu yoyote, nikiwa na akili timamu ninakubali kusoma katika Shule ya Sekondari ya Mvumi katika Tahasusi ya:……..na ninahidi kusoma na kujifunza kwa bidii na kufaulu kwa Alama…….(jaza kati ya hizo) **A,B,C** katika mazoezi,majaribio na mitihani yangu yote nitakayofanya shuleni ili niweze kufikia malengo yangu,ya shule na ya Taifa kwa ujumla. Pia ninaahidi kutojihusisha kwa aina yoyote kati ya makosa yaliyoainishwa na hata mengine yasiyoainishwa kwenye fomu ya kujiunga.
Mimi (Jina kamili la mwanafunzi)……

wa Kidato cha…….. Katika Shule ya Secondari Mvumi,

Nimesoma na kuelewa sheria na taratibu **zote** za shule na nakubaliana nazo, endepo nitazivunja niwajibishwe ipasavyo.

Saini ya mwanafunzi:…… tarehe:……

Mimi Jina la mzazi/mlezi) …… nimeridhia mwanagu asome Tahasusi aliyopangiwa ambayo ni……katika Shule ya Sekondari ya Mvumi. Vilevile, ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu. Ninakubaliana na sheria za shule na kanuni zake, nitalipa ada na michango ya shule kama ilivyoainishwa na kwa muda mwafaka (mapema) ili kuwezesha shughuli za shule ziweze kufanyika kama zilivyopangwa.

Nimesoma na kuelewa sheria na taratibu **zote** za shule na nakubaliana nazo, endepo mwanafunzi huyu atazivunja awajibishwe ipasavyo.

Saini ya Mzazi/Mlezi……Tarehe……..
Mimi (Jina kamili la Mzazi/Mlezi)……

wa S.L.P……. SIMU……..

Mzazi/Mlezi wa ……

Kidato cha……

DIOCESE OF CENTRAL TANGANYIKA
MVUMI SECONDARY SCHOOL
SHERIA/KANUNI ZA SHULE

1. **MUONGOZO WA SHERIA ZA SHULE**

Mwanafunzi anatarajiwa kuonyesha nidhamu ya hali ya juu kipindi chote atakachokuwepo shuleni. Hii ni pamoja na kuwaheshimu wafanyakazi wa jumuiya ya shule. Kanuni hizi zinalenga maeneo muhimu ya mwanafunzi kama malezi ya kimwili na kiroho, nidhamu binafsi, uwajibikaji, usafi, kujituma kitaaluma na ufanisi katika utamaduni na michezo.

2. **MUONEKANO WA MWANAFUNZI**

2:1:1 Sare ya mwanafunzi wakati wa vipindi vya darasani kidato cha Kwanza mpaka cha Nne.
Wasichana wanatakiwa kuvaa shati jeupe la mikono mifupi, sketi ya damu ya mzee na sweta la damu ya mzee, viatu vya ngozi vyeusi vya kamba na soksi ndefu nyeupe. Kwa wavulana shati jeupe la mikono mifupi, suruali ya bluu- nyeusi (dark blue), sweta la rangi ya blue- nyeusi (dark blue), viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na kisigino kirefu na sio raba na soksi ndefu nyeusi.

2:1:2 Sare ya mwanafunzi baada ya vipindi vya darasani kidato cha Kwanza mpaka cha Nne.
Wasichana watavaa gauni la rangi ya dark blue (solo) mikono mifupi lenye urefu unaozidi magoti, wavulana suruali ya khaki na shati la rangi ya damu ya mzee la mikono mifupi. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa viatu vya wazi au kandambili wakati akienda kwenye bwalo la chakula.

2:2:1 Sare ya mwanafunzi wakati wa vipindi vya darasani kwa kidato cha Tano na Sita.
Wasichana watavaa sketi ya kijivu yenye Marinda inayozidi magoti Kwa urefu, shati jeupe la mikono mirefu, viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu na pia sio raba. Soksi ndefu nyeupe na sweta la rangi ya kijivu. Kwa wavulana suruali ya rangi ya kijivu, shati jeupe la mikono mirefu, viatu vya ngozi vyeusi vya kamba (sio travota) na pia visivyo na kisigino kirefu, soksi ndefu nyeusi.

2:2:2 Sare ya mwanafunzi baada ya vipindi vya darasani kidato cha Tano na Sita.
Wasichana watavaa gauni la damu ya mzee (solo) mikono mifupi lenye urefu unaozidi magoti, na wavulana watavaa suruali nyeusi na shati la rangi ya damu ya mzee la mikono mifupi. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa viatu vya wazi au kandambili wakati akienda kwenye bwalo la chakula.

2:3. Nguo za michezo
Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa katika sare za michezo kwa usahihi siku za michezo kama zilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga na shule.

2:4. Mwanafunzi anatakiwa kuonekana nadhifu muda wote hii ni pamoja na kuchomekea shati na kung'arisha viatu.

2:5. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi zilizochanwa vizuri. Wasichana hawaruhusiwi kusuka wala kuweka dawa nywele. Wavulana hawaruhusiwi kunyoa kipara au mitindo yoyote.

2:6. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa hereni, bangili, kofia, kufuga kucha wala kupaka rangi, pia miwani isiyothibitishwa na daktari hairuhusiwi shuleni.

3:0. **MAHUDHURIO**

3:1. Wanafunzi wote wanalazimika kufika shuleni kuanzia siku ya kwanza, kama kuna sababu ya msingi ya kutofika kwa muda uliopangwa, mzazi au mlezi analazimika kutoa taarifa mapema shuleni kwa barua au simu.

3:2. Wanafunzi wanalazimika kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na nje ya darasa kila siku.

3:3. Kama mwanafunzi atashindwa kufika shuleni kwa tarehe iliyopangwa kwa sababu za ugonjwa, mzazi analazimika kuitaarifu shule kwa barua kupitia kwa Makamu Mkuu wa Shule.

3:4. Kama mwanafunzi hatokuwepo shuleni kwa sababu nyingine kama vile msiba, mzazi au mlezi wa mwanafunzi husika analazimika kuomba ruhusa kwa Mkuu au Makamu Mkuu wa Shule kabla ya mwanafunzi husika kuondoka shuleni.

3:5. Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa mwanafunzi ambaye hatahudhuria vipindi vyote shuleni bila kuwa na sababu za msingi. Hatua hizo kali ni pamoja na kufanya kazi nzito kwa wiki moja. Utoro uliokithiri utasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule. Kutokuwepo shuleni kwa muda mrefu kwa sababu za ugonjwa kutasababisha mwanafunzi husika kurudia mwaka.

3:6. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka katika eneo la shule kuanzia saa **1:00** asubuhi mpaka saa **8:30** mchana) isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkuu au Makamu Mkuu wa Shule, Mwalimu wa Zamu au Walezi wa mabweni. Wanafunzi wa kutwa wanaruhusiwa kuondoka shuleni baada ya saa 8:30 mchana isipokuwa siku za Jumatano wataondoka saa kumi na nusu baada ya kuhudhuria kipindi maalumu.

3:7. Wanafunzi wa bweni hawaruhusiwi kutoka nje ya shule kwa siku za kawaida za wiki isipokuwa kwa dharura za ugonjwa ambapo kibali maalumu hutolewa na walezi wao wa mabweni. Wanafunzi wa bweni wanaruhusiwa kutoka nje wiki la mwisho la mwezi kwa ajili ya kupata mahitaji yao mbali mbali. Wanafunzi wakiume wataruhusiwa siku ya Jumamosi na wasichana wataruhusiwa siku ya Jumapili kuanzia saa 8:00 mchana mpaka saa 11:45 jioni. Mwanafunzi atakayechelewa kurudi kwa muda sahihi hataruhusiwa tena kutoka nje ya shule kwa mwaka mzima pia atalazimika kufanya adhabu nyingine nje ya darasa kwa wiki moja. (Ruhusa hizo zimezuiliwa kwa muda mpaka hapo itakapoamuriwa vinginevyo).

4. **KUWAHI SHULENI**

4:1. Mwanafunzi analazimika kufika shuleni kwa muda sahihi, saa **1:00** asubuhi kwa kila siku za masomo. Mwanafunzi atakaechelewa kufika kwa muda sahihi ataadhibiwa. Wanafunzi wanatakiwa kukusanyika katika eneo la parade wakiwa kimya na kutengeneza mistari kulingana na vidato vyao.

4:2. Wanafunzi wanalazimika kufika parade ground bila kukosa mara baada ya masomo kwa ajili ya matangazo.

4:3. Wanafunzi wanalazimika kuhudhuria vipindi vyote kwa muda sahihi. Kama mwalimu hatohudhuria darasani, viongozi wa wanafunzi darasani wanatakiwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa Shule au Makamu wake baada ya dakika kumi za mwanzo kupita. Kama Mkuu na Makamu wake hawapo shuleni, Mwalimu wa Taaluma anatakiwa kupewa taarifa. Mwanafunzi kushindwa kuhudhuria masomo kwa muda sahihi utapelekea mwanafunzi husika kupewa adhabu nzito nje ya darasa kwa wiki zima.

5. **TABIA NJEMA**

5:1. Mwanafunzi analazimika kuwasalimia walimu na wafanyakazi wengine wa shule kwa lugha ya kiingereza.

5:2. Mwanafunzi anatakiwa kujiheshimu ipasavyo muda wote akiwa darasani; kusimama wakati mwalimu anapoingia darasani na kusalimia kwa kusema moto wa shule, mwanafunzi haruhusiwi kuweka mikono katika mifuko ya sketi au suruali wakati wakiongea na mtu mzima, mwanafunzi analazimika kunyanyua mkono wakati akiomba kujibu au kuuliza swali darasani na kuwa kimya wakati mwenzao anaongea au kuuliza swali darsani.

5:3. Mwanafunzi anaruhusiwa kutoka nje ya darasa wakati wa kipindi kama tu atapata ruhusa ya Mwalimu husika wa kipindi.

5:4. Mwanafunzi haruhusiwi kupewa kazi ya kuandika ubaoni na mwalimu isipokuwa tu kama uandikaji au uchoraji huo ubaoni utakuwa ni sehemu ya somo au njia ya kujifunza.

5:5. Mwanafunzi anaweza kwenda kwenye Ofisi ya Mkuu wa Shule, nyumba za Wafanyakazi wa Shule na Ofisi ya Walimu kama tu atapewa kibali na wahusika wa sehemu husika.

5:6. Wanafunzi wanapaswa kutumia lugha nzuri muda wote kwa Walimu, Wafanyakazi wengine wa Shule na kwa Wanafunzi wenzao.

5:7 Mwanafunzi anapaswa kuhakikisha kuwa kila mara yupo kwenye sehemu safi na sahihi. Mwanafunzi analazimika kuokota uchafu wowote ulio mahali pake na kuuweka kwenye dust bin za uchafu bila kujali uchafu huo umefikaje eneo hilo. Mwanafunzi atakaekutwa sehemu chafu ataadhibiwa.

5:8. Mwanafunzi akishindwa kufuata mwuongozo huo hapo juu kuhusu tabia njema anaweza kusimamishwa masomo kwa muda au kufukuzwa shule kutokana na uzito wa kosa husika.

6. **KUHESHIMU MALI ZA SHULE**

6:1. Mwanafunzi analazimika kuheshimu na kutunza mali za shule kwa muda wote atakaokuwa hapa shuleni, hairuhusiwi kuchora au kuandika maandishi kwenye kuta, madawati au meza za shule. Mwanafunzi analazimika kutunza majengo, vitabu na samani zote za shule.

6:2. Mwanafunzi haruhusiwi kuchukua kitu chochote mali ya shule kama vile vitabu, majarida au zana za kufundishia bila idhini ya Mwalimu au mtu husika wa vifaa hivyo. Kitendo hicho kitachukuliwa kama ni wizi na mwanafunzi husika ataadhibiwa kulingana na kosa la wizi.

6:3. Uharibifu wa makusudi wa mali za shule au vifaa vya wanafunzi wenzake kwa njia yoyote hautavumilika na itamlazimu mwanafunzi husika kulipa mali husika iliyoharibiwa na kuambatana na adhabu nyingine kutokana na kosa husika.

6:4. Kushindwa kuheshimu mali za shule kama ilivyoelezwa hapo juu kutasababisha mwanafunzi husika kulipa au kusimamishwa masomo au adhabu zote kwa pamoja kulingana na uzito wa kosa husika.

7. **MATUMIZI YA LUGHA YA KIINGEREZA SHULENI.**

7:1. Kiingereza ni Lugha ya kuongea na kuandika ya shule. Walimu na wanafunzi wanapaswa kutumia Kiingereza muda wote wawapo shuleni isipokuwa kama kuna tatizo la kutoelewana kati ya Mwalimu na Mwanafunzi.

7.2. Mwanafunzi akishindwa kufuata sheria hii ataadhibiwa ipasavyo.

8. **WAKATI WA KUONDOKA SHULENI**

Wanafunzi wote wanatakiwa kuingia na kutoka shule kupitia geti kuu la shule na sio vinginevyo. Mwanafunzi atakaye kamatwa akipitia njia ambayo sio sahihi ataadhibiwa.

9. **MAKOSA MENGINEYO**

9:1. Mwanafunzi haruhusiwi kutafuna chochote darasani.

9:2. Mwanafunzi haruhusiwi kutupa takataka ovyo.

9:3. Kamera haziruhusiwi shuleni isipokuwa kama kuna matukio maalumu shuleni kama vile sherehe za mahafali.

9:4. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki Vifaa vya umeme kama vile vichemshia maji, pasi, majiko ya umeme, vifaa vya muziki katika mazingira ya shule. Mwanafunzi atakaekamatwa na vifaa tajwa hapo juu vitachukuliwa na kuharibiwa na mwanafunzi husika ataadhibiwa ipasavyo.

10. **MAKOSA MAKUBWA YA KINIDHAMU**

10:1. Mwanafunzi anaweza kupewa adhabu ya kusimamishwa masomo kwa makosa makubwa ya kinidhamu, uamuzi wake utatolewa na Kamati ya Nidhamu ikishirikiana na Mkuu wa Shule.

10:2. Mwenyekiti wa Kamati ya Nidhamu baada ya kujadiliana na Bodi ya Shule wataamua kama mwanafunzi afukuzwe shule au la kutokana na utovu wa nidhamu uliokithiri. Kama mzazi au mlezi wa mwanafunzi aliyefukuzwa shule hajaridhika na adhabu hiyo anaruhusiwa kukata rufaa kwenye Bodi ya Shule, na Bodi hiyo ya Shule italishughulikia suala hilo katika vikao vyake vya kawaida.

10:3. **YAFUATAYO NI MAKOSA YANAYOWEZA KUMSIMAMISHA MWANAFUNZI MASOMO KWA MUDA AU KUFUKUZWA SHULE**

- Kusema uongo
- Udanganyifu
- Kutumia lugha ya matusi kwa Wafanyakazi wa Shule au Wanafunzi wenzake
- Kumshambulia Mfanyakazi au Mwanafunzi mwenzake
- Kuiba mali za shule au Wanafunzi wenzake
- Kuharibu mali za shule au Wanafunzi wenzake
- Uvutaji sigara au dawa za kulevya ikiwemo bangi na Pombe.
- Kujihusisha na mapenzi
- Kupata mimba au kusababisha mimba
- Kumiliki kisu au silaha yoyote ndani ya eneo la shule
- Kuanzisha migomo au fujo shuleni
- Kupatikana na kesi ya jinai.
- Utoro uliokithiri ikiwa ni pamoja na kutohudhuria vipindi darasani na shughuli nyingine za kila siku nje ya darasa.
- Kutoka katika eneo la shule usiku bila ruhusa kutoka kwa wahusika.
- *Mwanafunzi akikamatwa na Simu ya mkononi, simu itaharibiwa hadharani mbele ya wenzake na atasimamishwa masomo kwa mwezi mmoja, endapo atarudia kosa hilo mwanafunzi huyo atafukuzwa shule na simu kuharibiwa.
- *Tabia au vitendo vyote ambavyo vitashusha hadhi na kuchafua taswira ya shule hata kama vimefanyika nje ya mazingira ya shule.

MUHIMU

Baada ya kusaini fomu hii, mzazi au mlezi anashauriwa kubaki na nakala ya kivuli ya sheria za shule kwa kumbukumbu ili inapotokea mwanafunzi amefanya kosa iwe rahisi kwa mzazi/mlezi kujua uzito wa adhabu ya kosa husika.